



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAJI  
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TABORA  
(TUWASA)



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MAADHIMISHO YA WIKI YA MAJI TABORA TAREHE 16 – 22 MACHI, 2023**

Mhandisi Mayunga Kashilimu, Mkurugenzi Mtendaji TUWASA leo tarehe 16.03.2023 amewaarifu wakazi wa Tabora kuhusu Maadhimisho ya Wiki ya Maji mwaka huu yenye kauli mbiu **“Kuongeza kasi ya mabadiliko katika sekta ya maji kwa maendeleo endelevu ya uchumi”** kuwa TUWASA imeandaa promosheni ambazo zitaanza tarehe 16.03.2023 na kumalizika tarehe 15.04.2023.

Ameeleza promosheni hizo zitawahusu wateja wapya na wale waliositishiwa huduma kwa sababu ya madeni ya maji isipokuwa waliositishiwa maji kwasababu ya matumizi kinyume na taratibu.

**1. WATEJA WAPYA**

- Watalipia shilingi 150,000/= kwa mkupuo.
- Wakazi watakaohusika ni wote waliopo umbali wa mita 5 hadi 50 kutoka kwenye bomba kubwa la maji
- Mteja atalipia huduma baada ya kupimiwa na kukidhi sharti la umbali wa mita zisizozidi 50.

**2. WATEJA WALIOKATIWA MAJI KUANZIA JUNI 2022 KURUDI NYUMA.**

- Mteja hatalipia gharama ya kurejesha maji tshs 15,000/=
- Mteja atatakiwa kulipa nusu ya deni na deni litakalobaki atalipia kwa awamu nne hadi ifikapo Juni 2023.
- Wateja waliokatiwa maji wenye miundombinu ya maji iliyo haribika isiyozidi umbali wa mita 50 watatakiwa kulipa 150,000/= tu na kuwekewa miundombinu mipya ya maji.

Aidha ameeleza changamoto ya wizi wa Mita za maji ambapo takribani mita 200 zimeibwa na tayari vyombo vya Ulinzi na Usalama vinafanyia kazi changamoto hiyo.

Amewasisitiza wakazi wa Tabora kutumia vizuri fursa hii ya promosheni kwakuwa maji ni uchumi, maji ni maendeleo, maji ni amani.

Najibah B. Batenga

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma

16.03.2023